# CHUNGA KAZI NA **SAMAKI BIMA!**



## CONTACT US

for quotation request or any enquiries

+254 709 626 000
samakibima@gakenya.com
insure@gakenya.com
www.gainsuranceltd.com

SCAN ME FOR MORE DETAILS

Regulated by The Insurance Regulatory Authority

# SAMAKI BIMA

*Ni bima inayolinda ukulima wa samaki ulioko kwa maji au nchi kavu, kutokana na majanga kadha wa kadha.*

## Upana wa bima

- Vifo vya samaki kutokana na ajali, magonjwa, au kuondolewa kwa ushauri wa mtaalamu wa ufugaji wa samaki.
- Wizi wa samaki .
- Hasara kutokana na uharibifu wa nyavu au vizimba

## Aina ya samaki chini ya bima

- Ngege
- Kambale
- Trauti
- Sangara/Mbuta

## Bima haisimamii

- Vifo vya samaki kutokana na kutopewa lishe bora
- Hasara kutokana na kuharibika kwa nyavu, isipokuwa ikiwa vizimba pia vimeharibiwa na janga la hali ya hewa
- Hasara au vifo kutokana na kuvuna samaki walioko chini ya bima kuvunwa kabla ya mda wake
- Hasara ama vifo vilivyosababishwa moja kwa moja au kwa namna nyingine kutokana na vita, ugaidi, migomo, vurumai, ghasia na hujuma.
- Wizi wa samaki, vizimba, au nyavu uliofanywa na wafanyakazi au wanafamilia wa aliyechukua bima.

## Inachohitajika

- Fomu iliyojazwa kikamilifu
- Nakala ya nambari ya PIN kutoka KRA
- Nakala ya kitambulisho
- Wasifu (CV) ya meneja wa shamba la samaki
- Ripoti kutoka kwa Mtaalamu wa ufugaji wa samaki akihakikisha afya ya samaki na ukulima mzuri na unaofaa.

## Ili kupata bima hii, lazima mkulima atimize yafwatayo:

- Wakulima wa samaki wawe wenye leseni na waliosajiliwa na mamlaka husika Kitengo cha Usimamizi wa Fukwe (Beach Management Unit)
- Uzoefu wa angalau miaka miwili ya ukulima wa Samaki
- Mkulima lazima awe na rejesta ya lishe ya samaki
- Ukaguzi wa Samaki angalau mara moja kwa mwezi
- Usalama wa saa ishirini na nne kwa ufuo (Udhamini wa Mlinzi)
- Nyavu ziwe katika hali nzuri na zitumike kulingana na mipaka ya utumizi

## Namna ya kupata bima:

- Mpendekezaji anajaza fomu ya maombi
- GA watatoa masharti ya bima pamoja na bei (quotation)
- Mpendekezaji analipa ada ya bima (premium)
- Daktari wa mifugo/Mtaalamu wa ufugaji wa samaki atakagua shamba na atoeripoti kwa GA
- Cheti cha bima kitapewa mteja ili asahihishe yeye kuhakikisha amekubali masharti
- Kupeanwa kwa sera ya bima (policy document) kwa mmliki wa bima

